



# Mpango stahiki wa afya Kwa mtazamo

## NANI ANASTAHILI?

### WATU BINAFSI WALIO:

- Wakazi wa Jimbo la New York
- Marekani kihalali
- Hawastahiki kwa Medicaid, Mpango msingi au Child Health Plus

### WASILIANA NASI:

- [nystateofhealth.ny.gov](http://nystateofhealth.ny.gov)
- 1-855-355-5777 au TTY 1-800-662-1220

NY State of Health inazingatia sheria za haki za raia za Shirikisho zinazotumika na haibagui kwa msingi wa mbari, rangi, asili ya taifa, jinsia, umri au ulemavu katika mipango na shughuli zake za afya.

## NI NINI KINACHOSHUGULIKIWA?

- Huduma za bure za kuzuia maambukizi
- Huduma za wagonjwa waliolazwa
- Huduma za wagonjwa wasiolazwa
- Huduma za uzazi na watoto wachanga
- Huduma za dharura
- Maabara na upigaji picha
- Dawa za tiba
- Huduma za Utengenezaji Upya
- Huduma za afya ya kiakili na matatizo ya dawa za kulevya
- Huduma za usimamizi wa uzima wa mwili na magonjwa sugu
- Meno na uonaji kwa watoto

***Afya ya meno kwa watu wazima na faida nyingine zinaweza pia kushugulikiwa kwa mipango mingine.***

# MPANGO STAHIKI WA AFYA (QHP) INAGHARIMU PESA NGAPI?

**MALIPO YA BIMA YA KILA MWEZI:** Bei utakayolipa kila mwezi itategemea mpango utakaouchagua. Watu wengi wamehitimu kwa mikopo ya kodi ambayo hupunguza gharama yako ya kila mwezi. Watu wanaopata hadi \$48,240 kwa mwaka na familia ya watu 4 inayopata hadi \$98,400 huenda ikastahiki mikopo ya kodi.

**KUCHANGIA GHARAMA:** Uchangiaji wa gharama ni kiasi unacholipa wakati unapata huduma za afya. Watu wengine pia wanastahiki kupata msaada kulipa gharama hizi, kwa msingi wa mapato yao. Hapa chini pana mifano ya viwango vya uchangiaji wa gharama ya QHP kwa mipango ya kiwango inayotolewa katika ngazi nne. Mipango mingine inayopatikana na uchangiaji wa gharama tofauti na huduma za ziada zilizoshugulikiwa.

UCHANGIAJI WA GHARAMA KWA HUDUMA ZA AFYA	PLATINAMU	DHAHABU	FEDHA	SHABA
Kiwango kitakachokatwa Kila Mwaka	\$0	\$600	\$2,000	\$4,000
Huduma za Kuzuia Maambukizi	Bure	Bure	Bure	Bure
Ziara za Daktari za Huduma za Msingi	\$15	\$25	\$30	Uchangiaji wa gharama ya 50%
Ziara kwa Mtaalamu	\$35	\$40	\$50	Uchangiaji wa gharama ya 50%
Kiingilio kwa kila muda unaotumia katika Kulazwa Hospitalini	\$500	\$1,000	\$1,500	Uchangiaji wa gharama ya 50%
Ziara za Mgonjwa asiye wa Kulazwa wa Afya ya Kitabia	\$15	\$25	\$30	Uchangiaji wa gharama ya 50%
Ziara ya Wagonjwa Wanaolazwa wa Afya ya Kitabia kwa kila kiingilio	\$500	\$1,000	\$1,500	Uchangiaji wa gharama ya 50%
Chumba cha Dharura	\$100	\$150	\$250	Uchangiaji wa gharama ya 50%
Huduma ya Dharura	\$55	\$60	\$70	Uchangiaji wa gharama ya 50%
Tiba ya Kimwili, Tiba ya Usemi, Tiba ya Kikazi	\$25	\$30	\$30	Uchangiaji wa gharama ya 50%

UCHANGIAJI WA GHARAMA KWA DAWA YA TIBA	PLATINAMU	DHAHABU	FEDHA	SHABA
Mwigo	\$10	\$10	\$10	\$10
Bidhaa Inayopendelewa	\$30	\$35	\$35	\$35
Bidhaa ambayo Haipendelewi	\$60	\$70	\$70	\$70